HOTUBA YA RAIS WA CHAMA CHA WANASHERIA TANZANIA BARA (TANGANYIKA LAW SOCIETY) FELIX G. KIBODYA ALIYOITOA KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA SHERIA (LAW DAY) JUMATANO TAREHE 2 FEBRUARI 2011 - MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

Mheshimiwa Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Mhe. Mohamed Chande Othman, Jaji Mkuu wa Tanzania,
Mhe. Anne Makinda, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Mhe. Celina Kombani, Waziri wa Katiba na Sheria,
Wahe. Mawaziri mliopo,
Waheshimiwa Mabalozi,
Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Ya Rufani,
Waheshimiwa Majaji Wakuu wastaafu Augustine Ramadhani na Barnabas Samatta,
Mheshimiwa Spika Mstaaafu Pius Msekwa,
Mheshimiwa Jaji Kiongozi
Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania
Waheshimiwa majaji wastaafu Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu,
Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
Wastahiki viongozi wa Dini Mliopo,
Waheshimiwa Viongozi mliopo,
Viongozi wa Vyama vya siasa mliopo,
Mawakili wenzangu,
Mabibi na Mabwana!

Siku ya leo ni siku muhimu sana sio tu kwa majaji, mahakimu na sisi mawakili bali kwa Watanzania wote. Sherehe hii ni kiashiria kinachoonesha umuhimu wa

mhimili wa mahakama katika jamii hususan kuhusiana na utawala wa sheria kama inavyobainishwa ndani ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Rais,

Kuna Msemo unaofahamika na wengi usemao: ***kutokuijua sheria siyo utetezi*** (yaani ignorance of law is no defense). Ingawaje msemo huu una nguvu ya kisheria, lakini kwa kiasi kikubwa sana ni wa kinadharia. Heby tujiulize, hivi ni Watanzania wangapi wanaozifahamu sheria hasa zile za jinai na zile zinazobainisha haki zao za Msingi? Sina shaka jibu la swali hili ni rahisi nalo ni kwamba ni watu wachache sana - tena hata hao wachache - wanazijua sheria hizo kupitia kwa wanasheria.

Kwa hiyo basi, kama sheria itaendelea kuwa bidhaa adimu hapa nchini, ni dhahiri kuwa Watanzania walio wengi na hasa wa vijijini, hawana kabisa, ama hata kama wanao, basi wana ufahamu mdogo sana wa jinsi mahakama zetu zinavyofanya kazi. Mapungufu haya ya kimsingi yana athari ya moja kwa moja katika demokrasia, amani na utulivu nchini kwani kama wananchi walio wengi na hasa wanyonge hawana uelewa wa sheria zinazotungwa na wawakilishi wao na jinsi mahakama zinavyofanya kazi yake, dhuluma, uvunjifu wa amani na madhila mengine yanayofanana na hayo hayatakosekana katika jamii. Hii ni hatari kwa Taifa changa kama Tanzania linalojitutumua kuisimika na kuikuza demokrasia.

Mheshimiwa Rais,

Mfano halisi wa uelewa mdogo wa sheria ninaoweza kuutoa leo hii ni mjadala wa katiba mpya ulioibuka hivi karibuni na ambao baadhi ya wanasiasa wameanza kuuhodhi. Ukiwauliza wananchi wa kawaida kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watakwambia kuwa kwa hakika, wananchi wamechoshwa nayo kwa hiyo wanahitaji Katiba mpya. Lakini ukiwauliza mapungufu ya Katiba iliyopo hawana jibu wala hoja yeyote bali, kwa haraka sana, watakwambia kuwa wameambiwa na wanasiasa waliobobea kuwa katiba iliyopo haifai ingawaje wao hawajaiona wala kuisoma! Huu ni mfano mdogo unaodhihirisha kutokuwepo uelewa

wa maswala ya sheria na vyombo vilivyopewa dhamana ya kusimamia haki hapa nchini.

Mheshimiwa Rais,

Maudhui ya Siku ya Sheria mwaka huu ni "UMUHIMU WA ELIMU KUHUSU MAHAKAMA KAMA HATUA YA MSINGI YA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA JAMII" Na tujiulize basi, ni nani mwenye jukumu la kutoa elimu kwa jamii? Haiyumkini serikali ndiyo yenye jukumu la Msingi la kutoa elimu ya sheria na vyombo vya utoaji haki kwa wananchi. Kwa maantiki hiyo, Wizara ya Katiba na Sheria ina wajibu wa kubuni mikakati ya kutoa elimu ya sheria kwa umma kupitia idara yake ya utoaji msaada wa sheria na ile ya elimu kwa umma, kama ipo.

Ingawaje serikali ndiyo yenye jukumu la Msingi katika kutoa elimu ya sheria kwa umma, nachelea kusema kuwa Idara ya Mahakama haiwezi kujivua kabisa jukumu hilo. Nakumbuka miaka ya nyuma, kilikuwepo kipindi cha redio kiitwacho "***Ijue Mahakama Yako***" kilichokuwa kikirushwa hewani na iliyokuwa Radio Tanzania wakati ule. Sina uhakika kama kipindi hicho bado kinaendelea tena kwa kasi ileile. Ni rai yangu, kupitia kwa Mhe. Jaji Mkuu kuwa, Idara ya Mahakama itauangalia upya utaratibu huo hasa ikizingatia kuwepo kwa vyombo lukuki vya utangazaji vinavyoweza kuwafikia wananchi walio wengi tena kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Rais,

Je, ni nini wajibu wa Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara (TLS) katika utoaji wa elimu ya sheria kwa Umma? Chama chetu kina mawakili/wanachama takriban 1,500 hivi sasa. Kitakwimu, Mwanasheria mmoja anahudumia wananchi wapatao 27,000. Takwimu hizi haziwiani kabisa na zile za majirani zetu katika Jumuiya ya Afrka Mashariki. Kwa mfano, Kenya ina mawakili wapatao 7,000. Wakili mmoja anahudumia wakenya wapatao 6,000. Uganda ina mawakili 1,400 ambapo wakili mmoja anahudumia waganda wapatao 9,000.

Kutokana na takwimu nilizozianisha hapo juu, ni dhahiri kuwa jukumu la utoaji elimu ya sheria kwa umma ni letu sote. Nafurahi kutoa taarifa kuwa Chama cha Wanasheria Tanzania bara kimekuwa mstari wa mbele kutoa elimu ya sheria kupitia kamati ya msaada wa sheria. Kwa mujibu wa kanuni tulizojiwekea, kila wakili anawajibika kutoa msaada wa sheria kwa mhitaji. Msaada huo unaweza kuwa ushauri wa sheria, msaada wa kufuatilia haki ya mhitaji katika mamlaka husika au kufungua shauri mahakamani. Kupitia utaratibu huu, Chama chetu kimebaini kuwa sio tu Watanzania wengi hawazifahamu sheria, bali hawajui kabisa ni wapi wapeleke madai yao ili yapate ufumbuzi.

Vilevile, Chama chetu kinashirikiana kwa karibu sana na wadau wengine wanaojihusisha na utoaji wa msaada wa Sheria. Chini ya uongozi wa Chama Chetu kupitia mpango wa maboresho ya sekta ya sheria, tupo mbioni kukamilisha utaratibu utakaorahisisha uratibu wa shughuli za utoaji msaada wa sheria nchini.

Mheshimiwa Rais,

Kuanzia mwaka 2007, Chama chetu kiliamua kutenga siku moja ya Msaada wa Sheria kitaifa. Mwaka jana siku ya msaada wa sheria iliadhimishwa katika mikoa kumi ya Tanzania bara. Kitaifa, shughuli hii iliadhimishwa mwezi Novemba mjini Dodoma ambapo mgeni rasmi alikuwa Mhe. Celina Kombani, Mbunge, Waziri wa Katiba na Sheria. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza serikali yako kwa kufadhili siku ya msaada wa sheria kwa miaka minne sasa, kwa kifupi toka ilipoanzishwa.

Mheshimiwa Rais,

Pamoja na juhudi nilizozitaja za kuelimisha jamii, safari bado ni ndefu. Kwa mfano, watu wengi hawana uelewa wa kuwepo vyombo vya kutatua migogoro vilivyoundwa nje ya muundo wa Mahakama (yaani specialized tribunals). Vyombo hivyo vina majukumu mahsusi na ambayo yanahitaji maamuzi ya haraka. Ni muhimu kwa wananchi wakazifahamu na hatimae kuvitumia vyombo hivyo muhimu.

Mheshimiwa Rais,

Kuwepo kwa uelewa mdogo wa shughuli za mahakama kumejenga taswira potofu miongoni mwa jamii. Kwa mfano, wengi wetu tumesikia kuwa mahakama zimegubikwa na tuhuma za rushwa na ambazo zinawagusa pia mawakili. Inawezekana tuhuma hizo zisiwe sahihi lakini pengine taswira hizo zinatokana na kutokuwepo kwa uwazi au ueledi.

Kwa maoni yetu, ili kuondoa taswira hizo potofu, kwanza kabisa mahakama inabidi ijiweke karibu zaidi na jamii pamoja na mihimili mingine ya dola bila kuathiri uhuru wake. Kwani siyo sahihi kwa chombo muhimu kama mahakama kujiwekea uzio utakaowanyima uwezo wa kutambua mambo yanayoendela katika jamii iwe katika Nyanja ya uchumi, siasa au jamii. Kwa kifupi wayafahamu mahitaji na matarajio ya jamii.

Pili, ili Mahakama iweze kufanya klazi yake ya utoaji haki, si budi serikali iiwezeshe. Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi zako zinazolenga kuboresha shughuli za idara ya mahakama hasa kwa kuteua majaji wengi zaidi kuliko awamu zilizokutangulia. Tunataraji kuwa kukamilika kwa mpango wa maboresho ya seka ya sheria kutazaa matunda maridhawa.

Tatu, Mambo mengine pengine ni ya kimtazamo zaidi kuliko rasilmali. Kwa mfano, ukiangalia kasi ya ujenzi wa madarasa, vituo vya afya na hata ofisi za watendaji wa vijiji utaona kuwa haziendani kabisa na kasi (kama ipo) ya ujenzi wa mahakama hasa za mwanzo na wilaya. Kwa hiyo basi ni muhimu sana serikali ikabuni mikakati ya kuwanoa watendaji wa ngazi zote ili wabadili mtazamo uliojengeka kwa miongo mingi sasa wenye dhana ya kuwa idara ya mahakama haipaswi kuingiliwa wala kuhusiswa na mihimili mingine ya dola.

Mheshimiwa Rais,

Mwisho kabisa, naomba kuchukua nafasi hii kutambua mchango muhimu wa Serikali kupitia mradi wa maboresho ya sheria, kwa kuanzisha mchakato wa kubuni Sera ya

Msaada wa Sheria. Pindi Sera hii itakapokamilishwa na kutungiwa sheria, itasaidia kwa kiasi kikubwa kusambaza elimu ya sheria kwa Watanzania. Ni rai yetu kuwa mchakato huu ulioanza zaidi ya mwaka moja sasa utahitimishwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Rais,
Mheshimiwa Jaji Mkuu,
Naomba kuwasilisha!